TANGAZO LA SERIKALI NA. 843 la tarehe 02/10/2020

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA

(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*Zimetungwa chini ya kifungu cha 7(1) na 16(1)*

## MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO ZA ADA NA USHURU ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA ZA MWAKA 2020

SEHEMU YA KWANZA

UTANGULIZI

Jina Tangazo la Serikali Na.278 la mwaka 2017

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Marekebisho ya Sheria Ndogo za Ada na Ushuru za Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa za Mwaka 2020 na zitasomwa pamoja na Sheria Ndogo za Ada na Ushuru za Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa za Mwaka 2017 ambazo zitajulikana kama Sheria Ndogo Kuu.

Marekebisho ya Jedwali

2 Sheria Ndogo kuu zinarekebishwa kwa;

(a) kufuta sehemu B(b) ya Jedwari; na

(b) kufuta sehemu "D" na kuiandika upya kama ifuatavyo;

SEHEMU D

*"Ada na Ushuru wa mazao ya kilimo kwa ujazo wa kuanzia tani moja"*

| Na. | Aina ya mazao | Kiwango |
|---|---|---|
| 1 | Viazi | Asilimia tatu (3%) ya bei ya kununulia |
| 2 | Kabichi | Asilimia tatu (3%) ya bei ya kununulia |
| 3 | Karoti | Asilimia tatu (3%) ya bei ya kununulia |
| 4 | Ufuta | Asilimia tatu (3%) ya bei ya kununulia |
| 5 | Mchele | Asilimia tatu (3%) ya bei ya kununulia |
| 6 | Maharage | Asilimia tatu (3%) ya bei ya kununulia |
| 7 | Kahawa iliyokobolewa | Asilimia tatu (3%) ya bei ya kununulia |
| 8 | Pareto | Asilimia tatu (3%) ya bei ya kununulia |

*Tangazo Namba 843 (Linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| 9 | Vitunguu swaumu | Asilimia tatu (3%) ya bei ya kununulia |
| 10 | Vitunguu maji | Asilimia tatu (3%) ya bei ya kununulia |
| 11 | Nyanya | Asilimia tatu (3%) ya bei ya kununulia |
| 12 | Mahindi/Alizeti/ngano/Mtama | Asilimia tatu (3%) ya bei ya kununulia |
| 13 | Mazao yasiyotajwa | Asilimia tatu (3%) ya bei ya kununulia |

3. Sheria Ndogo kuu zinarekebishwa kwa kufuta sehemu F ya Jedwali na kuiandika upya kama ifuatavyo;

## SEHEMU F

## ADA AU USHURU WA SHUGHULI ZA BURUDANI, UTAMADUNI, SANAA NA MATANGAZO

| NA | AINA YA HUDUMA | KIWANGO CHA ADA AU USHURU |
|---|---|---|
| 1 | Washereheshaji | 15,000/= kwa siku |
| 2 | Wapambaji wa kumbi za burudani ( harusi, sherehe za jikoni, sherehe za kuaga binti na nyinginezo) | 15,000/= kwa siku |
| 3 | Mtoa burudani (DJ) | 15,000/= kwa tukio |
| 4 | Wamiliki wa kumbi mbalimbali | -ukumbi unaochukua watu 100-200 shilingi 20,000/=kwa siku<br>-ukumbi unaochukua watu 300-500 shilingi 40,000/= kwa siku |
| 5 | Matangazo ya barabarani ya sherehe | 20,000/= kwa tukio moja kwa siku |
| 6 | Wapishi wa vyakula | 30,000/= kwa tukio moja kwa siku |
| 7 | Picha jongevu na mnato | 15,000/= kwa tukio moja kwa siku. |
| 8 | Matangazo ya kuuza bidhaa zinazopungua bei (promotion) | 30,000/= kwa tangazo |
| 9. | Maombi ya kibali cha kufanya Tiba za Jadi | 20,000/= kwa siku |
| 10. | Matamasha | 30,000/= kwa tamasha |
| 11. | Fete na bahati nasibu | 20,000/= kwa siku |
| 12. | Mnada | 30,000/= kwa mnada |
| 13. | Kupiga muziki ukumbi mkubwa | 50,000/= kwa siku |
| 14. | Kupiga muziki ukumbi mdogo | 30,000/= kwa siku |
| 15. | Matangazo ya Biashara kwa kutumia vipaza sauti; au vipeperushi; au | 30,000/= kwa siku. |

*Tangazo Namba 843 (Linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| | vitambaa na; au fani za sanaa ambazo hazijatajwa hapo juu. | |

*Ada zote katika sehemu ya XII (1)-(7) zitalipwa kwa pamoja na mwenye sherehe.*

4.Sheria Ndogo Kuu inafanyiwa marekebisho katika sehemu G Ada na Ushuru wa stendi, maegesho ya vyombo vya usafiri Ushuru wa Maegesho ya vyombo vya usafiri kwa kuongeza:-

i) Pikipiki na Bajaji………………………10,000/= kwa mwaka

5.Sheria Ndogo Kuu inafanyiwa marekebisho katika Jedwali Sehemu I kwa kufuta baadhi ya vifungu na kurekebisha baadhi ya vifungu kama ifuatavyo;

SEHEMU I

ADA NA USHURU WA MAZAO YA MALIASILI

*Aina ya zao* *Kiwango cha ushuru (Tshs)*

a) Sehemu I (b) ushuru wa Tshs.2,000/= wa mkaa inarekebishwa na kuwa Tshs.650/= kwa gunia la kg50.
b) Ada ya usajili wa biashara ya mazao ya misitu sehemu I (h) inafutwa.
c) Sehemu I (l) ada ya usajili ya mashine za kukatia miti inarekebishwa na kuwa Tshs.50,000/= kwa mwaka.
d) Sehemu I(y) tozo ya ada kwa mazao ya miti ya asili inayovunwa kwenye misitu ya hifadhi na ardhi ya kawaida kwa $M^3$ isipokuwa miti aina ya *sandal* inafutwa na badala yake itatozwa 5% ya mrahaba wa tozo ya Mamlaka ya Misitu Tanzania.

*Tangazo Namba 843 (Linaendelea)*

Lakiri ya Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio la Mkutano wa Baraza la Madiwani uliofanyika katika Ukumbi wa Halmashauri tarehe 27 ya mwezi Julai, 2019 mbele ya:-

SUNDAY NDORI DEOGRATIUS,
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa*

EDWARD LESLIE HAULE,
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa*

NAKUBALI,

…………………………………….……
SELEMANI S. JAFO (MB)
Waziri Ofisi ya Rais (TAMISEMI)

DODOMA,
Tarehe 02 Septemba 2020